Maswali

1. Mbona Farao mgeni aliogopa Waisraeli?
2. Farao alifanya Waisraeli wafanye nini?
3. Farao aliweka sheria gani katili?
4. Nani alipata mtoto mvulana?
5. Waliweka mtoto namna gani kwa miezi 3.
6. Baadaye Yokebedi alifanya nini iliyosaidia mtoto wao kuwa salama?
7. Nani alichunga mtoto?
8. Nani alipata mtoto?
9. Miriamu alifanya nini?
10. Bintiye Farao aliita mtoto nani? Hilo jina lina maana gani?

Majibu

1. Waisraeli walikuwa taifa kubwa.Farao aliogopa kwa sababu wanaweza kufanya vita naye.
2. Farao alifanya Waisraeli watumwa. Walimjengea miji.
3. Farao aliamrisha watoto wavulana wote wauwawe.
4. Amramu na Yokebedi walipata mtoto mvulana.
5. Walimficha kwa miezi 3.
6. Yokebedi alitengeneza kikapu cha manyasi. Alificha huyo mtoto wao kando ya mto ndani ya kikapu cha manyasi.
7. Miriamu alichunga mtoto.
8. Bintiye Farao alipata mtoto.
9. Miriamu aliuliza kama angeleta yaya. Alileta mama yake.
10. Binti huyo aliita mtoto Musa, maana yake ni tolewa nje.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1

16 Kuzaliwa kwa Musa

Kwa Biblia Kutoka mlango wa 1 na mlango wa 2: 1-10

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hataki watu wawe katili. Mungu analinda watu wake.

Somo

Watu 70 wa familia ya Yakobo walikaa Gosheni katika nchi ya Misri. Waliishi huko kwa miaka mingi. Walikua na kukuwa taifa kubwa sasawa na vile Mungu alikuwa ameahidi Yakobo. Waliitwa watu wa Israeli au Waisraeli. Israeli ni jina mpya Mungu alimpa Yakobo.

Kulikuwa na vita Misri. Farao aliyefanya Yusufu mtawala alishindwa. Kulikuwa na Farao mgeni asiyejua lolote kuhuzu Yusufu. Farao mgeni aliogopa alipoona taifa kubwa la Israeli lililokaa Gosheni. Aliogopa kwamba wanaweza kupigana naye. Aliamua kuwazuia waziwe na nguvu kamwe.

Kwanza aliwafanya wawe watumwa. Akawawekea wasimamizi. Waisraeli walipofanya kazi kwa ulegevu wasimamizi waliwapiga. Farao alifanya Waisraeli wajenge miji mikubwa yenye kuta kubwa mno. Pia walimjengea miji yake binafsi ya usalama na labda hata haram (piramindi).

Waisraeli walifanya kazi sana. Lakini waliendelea kuwa wengi. Waliendelea kuwa na nguvu. Farao alikuwa na wasi wasi. Alikuwa mtu katili. Aliweka sheria katili sana. Farao aliamrisha kwamba watoto wavulana wote wanaozaliwa na Waisraeli lazima wauwawe. Farao alifikiria kwamba watoto wavulana wasipozaliwa, hakutakuwa na wanaume wakukua na wapigane naye.



Farao alifanya Waisraeli wawe watumwa. Walifanya kazi nyingi ya kujenga miji. Picha hii ilipatikana kwa baadhi ya michoro ndani ya makaburi ya Misri.

Amramu na Yokebedi walikuwa na wasi wasi. Walikuwa na mwana aliyeitwa Haruni na binti aliyeitwa Miriamu. Yokebedi alikuwa anatarijia mtoto mwingine. Ikiwa atakuwa mvulana Farao atamua.

Yokebedi alizaa mtoto mvulana. Alikuwa mtoto mzuri sana. Yokebedi na familia yake hawakutaka auwawe. Walificha huyo mtoto. Walimficha kwa miezi mitatu. Lakini mtoto alianza kulia kwa sauti ya juu. Yokebedi alijua kwamba hivi karibuni, askari wa Farao watamsikia. Watapata mtoto na watamua.

Yokebedi alitaka kuokoa mtoto. Hawangeendelea kumficha kwa nyumba. Haingewezekana. Yokebedi alikuwa na shauri. Alienda kwa Mto wa Nile. Yokebedi alitafuta manyasi.

Akatengeneza kikapu cha manyasi, akapaka lami na sifa ili maji yasiingie ndani. Yokebedi akafunga mtoto wake mzuri nguo vizuri na kumbeba. Akaenda na bintiye Miriamu polepole mpaka Mto wa Nile.



Yokebedi alimbusu mtoto na akamueka kwa kile kikapu. Akamficha kwa manyasi kando ya Mto wa Nile. Miriamu alichificha karibu ili aone kitakachotokea. Miriamu alikuwa na wasi wasi ikiwa mtu atakuja na amchukue ndunguye mdogo.

Bintiye Farao alienda kuoga mtoni. Aliona kikapu kwa manyasi. Wajakazi wake walienda kuchukua kile kikapu. Bintiye Farao alipofungua kikapo mtoto alianza kulia. Huyu binti alihurumia mtoto. Alijua mtoto huyu alikuwa Mwisraeli. Aliamua kuchukua mtoto na awe wake.

Miriamu aliogopa sana. Nini kitafanyika kwa nduguye mdogo? Aliwaza haraka. Akakimbia kwa binti Farao. Akamuuliza, “Niende nikuletee yaya wa kukulelea mtoto?” Alifurahi aliposikia bintiye Farao akisema. “Ndiyo, enda.” Miriamu alikimbia haraka na kuleta Yokebedi.

Bintiye Farao alimpa Yokebedi mtoto. Alimwambia, “Chukua mtoto huyu na unilelee, nitakulipa kwa hayo malezi.”

Kwa hivyo Yokebedi akarudi nyumbani na mtoto - na alilipwa kwa kumlea. Mungu alikuwa amejibu maombi yao na mtoto wao ako sawa. Huyu binti wa Farao aliita mtoto ‘Musa,’ maana yake ‘tolewa nje.’ Alimuita **Musa** kwa sababu **alitolewa nje** ya mtoni.

Mungu alikuwa amemchagua Musa awaokoe Waisraeli kutoka Misri atakapokua wa umri. Mungu alifanya haya yote ili Musa aokolewe. Yokebedi hangeokoa Musa. Alimuacha kwa manyasi. Lakini kwa Mungu yote yawezekana. Mungu alipanga kila kitu kwa njia ya maajabu. Iliwezekana Yokebedi alee mtoto wake akiwa mchanga.